**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)**

*Unapojibu tafadhali taja:*
**Kumb. Na. AB. 50/65/01/41** **Tarehe: 19.09.2024**

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi,
Vyama vya Ushirika,
**TANZANIA BARA**

**Yah: UFAFANUZI WA BARUA YA MRAJIS KWA VYAMA VYA USHIRIKA KUHUSU ADA ZA UKAGUZI ZINAZOTOZWA NA COASCO**

Tafadhali husikeni na somo tajwa hapo juu.

2. Shirika limeona kwenye mitandao ya kijamii barua iliyotumwa kwenu ikihusu "**Malipo ya Ada za Ukaguzi wa Nje kwa Vyama vya Ushirika Unaofanywa na COASCO**", yenye kumbukumbu namba BA.28/69/01A/15 ya tarehe 17 Septemba 2024. Barua hiyo imeeleza kuwa, pamoja na mambo mengine, vyama vya ushirika vimekuwa vikilalamikia mabadiliko ya ada za ukaguzi zinazotozwa na COASCO, ikieleza kuwa ada hizo zinaweza kuathiri shughuli za maendeleo na ustawi wa vyama. Hivyo, inavielekeza vyama vya Ushirika kulipa ada iliyotozwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwenye ukaguzi wa mwaka 2024/25. Aidha, barua hiyo imeeleza kuwa yapo mazungumzo kati ya COASCO na TCDC yanayoendelea kuhusu suala hilo.

3. Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) ni Shirika la umma lililoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 15 ya mwaka 1982, na kufanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 2005. kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria tajwa, Shirika hili lina jukumu la kufanya ukaguzi na kutoa ushauri kwa vyama vya ushirika nchini. Aidha, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeanzishwa kwa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, kwa lengo la udhibiti/usimamizi na uhamasishaji wa vyama vya ushirika nchini, kama ilivyo ainishwa kwenye kifungu cha 8 cha Sheria hiyo. Kwa msingi huo, taasisi hizi mbili ni huru na zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria za kuzianzisha pasipo ya kuingiliwa na taasisi nyingine katika kutekeleza majukumu yake. Hivyo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika hana mamlaka ya kisheria ya kuingilia utendaji wa COASCO kwa kuelekeza Vyama vya Ushirika kiasi cha ada ya ukaguzi kinachopaswa kulipwa kwa COASCO kama ilivyo kwenye barua yake.

4. Ada za ukaguzi zinazotozwa na COASCO ni kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria Na. 15 ya mwaka 1982, iliyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 2005, (The Cooperative Audit and Supervision (Amendment) Act, 2005) ikisomwa pamoja na miongozo ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na miongozo ya ndani ya Shirika iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Viwango vya ada zinazotozwa huzingatia mawanda ya ukaguzi, ukubwa wa kazi, utaalam unaohitajika, muda, vihatarishi, na muhimu zaidi, uwezo wa chama kulipa ada husika. Baada ya ukokotoaji wa ada hizo, Shirika (Mkaguzi) huziwasilisha kwenye kikao cha pamoja na Bodi ya chama husika kwa ajili ya majadiliano na makubaliano kwa kuwa Bodi ya chama ni chombo huru katika kufanya maamuzi yanayohusu ustawi na uimara wa chama cha ushirika kwa kuzingatia misingi ya Kisheria kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 3(a) na (d) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni ya 51(a) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015. Makubaliano hayo ya kiwango cha ada huwekwa rasmi kwenye mkataba wa makubaliano ya ukaguzi (Engagement Letter) ili kufanya utekelezaji kuwa wa kisheria kwa mujibu wa taratibu za ukaguzi wa hesabu.

5. Kuanzia Julai 1, 2024 hadi sasa, Shirika limekamilisha ukaguzi kwa vyama vya ushirika 570. Vyama hivyo viliingia makubaliano na Shirika juu ya viwango vya ada ya ukaguzi na kufanya malipo kwa mujibu wa makubaliano hayo. Hata hivyo, Shirika halijapokea malalamiko yoyote kwa maandishi kutoka kwa vyama hivyo kuhusu viwango vya ada wanayopaswa kulipa. Aidha, Shirika linaendelea na zoezi la ukaguzi kwa Vyama Vikuu na AMCOS ambapo limepanga kukagua vyama 1,228 ifikapo tarehe 30 Septemba, 2024.

6. Gharama halisi ya ukaguzi hujulikana baada ya kuwasilishwa kwa rasimu ya hesabu za chama kwa kwa ajili ya ukaguzi wa mwaka husika. Endapo kiwango kilichoafikiwa kwa ajili ya kugharamia ukaguzi huo kinatofautiana na makisio yaliyopitishwa na wanachama kwenye mkutano mkuu, Vyama vinashauriwa kuomba makisio ya nyongeza (Suplementary budget) kwa mujibu wa Kanuni ya 62 (3) ya Kanuni za vyama vya Ushirika za mwaka 2015, tangazo la Serikali namba 272, 2015 kwa kuwa ukaguzi ni takwa la kisheria.

7. Hata hivyo, mpaka sasa hakuna mazungumzo yoyote yanayoendelea kati ya ofisi ya Mrajis na COASCO kuhusu utozaji wa ada za ukaguzi kama ilivyoelezwa kwenye barua yake. Hivyo, tunavishauri vyama kuendelea kulipa ada za ukaguzi kwa ukamilifu kama ilivyo kwenye mikataba wa makubaliano ya ukaguzi yaliyoafikiwa au yatakayoafikiwa kwenye zoezi la ukaguzi linaloendelea ili kuepusha usumbufu wa kuchelewa kwa zoezi la ukaguzi, upatikanaji wa taarifa kwa wakati, ujazaji wa ritani za kodi na uwasilishaji wa taarifa kwenye mikutano mikuu.

Nawatakia utekelezaji mwema,

Pamoja tujenge Uchumi,

CPA J.J. Mugeta
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

**Nakala:** Katibu Mkuu,
Wizara ya Kilimo,
Mji wa Serikali –Mtumba,
S.L. P. 2182,
**DODOMA.**

Mrajis wa Vyama vya Ushirika,
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania,
S. L. P. 201,
**DODOMA.**

Wakaguzi wa Ushirika Mikoa,
COASCO,
**TANZANIA BARA.**

Mwenyekiti,
Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC),
S. L. P. 2567,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,
SCCULT,
S. L. P. 20640,
**DAR ES SALAAM.**